Australian Government

COVID-19 VACCINATION

# Kwa nini mwajiri wangu katika huduma ya kutunza ananiuliza kama nimepokea chanjo ya COVID-19?

Taarifa ni ya sasa kwa tarehe 4 Juni 2021

Kuchanjwa ni kinga bora zaidi dhidi ya ugonjwa wa COVID-19. Kuwalinda wakazi katika huduma za wazee na wafanyakazi wanaowatunza ni kipaumbele.

Ndiyo maana ni muhimu kwa serikali na watoa huduma za wazee katika makazi yao kuelewa ni wafanyakazi wangapi wa huduma za wazee wameshachanjwa dhidi ya COVID-19. Habari hii husaidia kuelewa hatari kwa wakazi na wafanyakazi kuandaa, kupanga na kukabiliana na mlipuko wa COVID-19.

Ikiwa kuna mlipuko wa COVID-19 katika kituo chako, itakuwa muhimu kujua ni wafanyakazi wangapi wamechanjwa ili hatua za kinga ziweze kutolewa kwa wale ambao hawajachanjwa bado.

Rejesta ya Chanjo ya Australia inarekodi historia ya chanjo ya kila mtu. Lakini haijumuishi taarifa kuhusu kazi unayofanya au mwajiri wako.

Serikali ya Australia inaanzisha chombo kipya cha kuripoti kwa watoa huduma walioidhinishwa wa huduma za makazi ya wazee, na huduma za utunzaji wa wazee wa nyumbani na jamii, kwa kusudi hili. Sasa inapatikana kwa watoa huduma kutumia kwa misingi ya hiari kupitia Huduma Yangu ya Wazee (My Aged Care).

Wakati kuripoti ni hiari mwanzoni, watoa huduma walioidhinishwa wanahimizwa sana kuanza kutoa taarifa za kila wiki sasa hivi juu ya:

- jumla ya idadi ya wafanyakazi katika kila huduma ya wazee wa makazi
- jumla ya idadi ya wafanyakazi katika kila huduma ambao wamepata dozi moja ya chanjo ya COVID-19
- jumla ya idadi ya wafanyakazi katika kila huduma ambao wamepokea dozi zote zinazohitajika za chanjo ya COVID-19.

Kuanzia tarehe 15 Juni 2021, kuripoti kutakuwa sharti la lazima kwa watoa huduma walioidhinishwa wa huduma za wazee wa makazi. Kwa huduma za utunzaji wa nyumbani na jamii itakuwa sharti rasmi katika wiki zijazo.

## Je, hii inaniathiri vipi?

Mahali pako pa kazi patajadiliana nawe jinsi watakavyokusanya na kutoa taarifa juu ya idadi ya wafanyakazi katika kituo ambao wamepokea dozi moja ya chanjo ya COVID-19 na wale ambao wamepokea dozi zote zinazohitajika za chanjo ya COVID-19.

Ni muhimu ujue kuwa kupata chanjo ya COVID-19 ni ya hiari. Ni chaguo lako juu ya kuamua kupata chanjo au kutopata chanjo. Ni chaguo lako kumjulisha mwajiri wako ikiwa umepata au bado hujapata chanjo ya COVID-19. Ni muhimu pia kuelewa sababu habari hii inakusanywa ni kukinga wale unaowatunza.

### Je! Ni habari gani ambazo mahali pangu pa kazi panaweza kukusanya na kuripoti?

Ukusanyaji wa takwimu unafanana sana na jinsi mwajiri wako kwa sasa anavyorekodi taarifa za idadi ya wafanyakazi ambao wamepata chanjo ya mafua.

Mahali pako pa kazi patatoa taarifa zifuatazo kwa Idara ya Afya:

- jumla ya idadi ya wafanyakazi katika kila huduma ya wazee wa makazi
- jumla ya idadi ya wafanyakazi katika kila huduma ambao wamepata dozi moja ya chanjo ya COVID-19
- jumla ya idadi ya wafanyakazi katika kila huduma ambao wamepokea dozi zote zinazohitajika za chanjo ya COVID-19.

Taarifa ya ripoti zako za mahali pa kazi hazitamtambua mtu yeyote.

Kutoa taarifa kutajumuisha watu wote (pamoja na wanaojitolea) wanaofanya kazi katika kituo cha makazi ya wazee ambao wanawajibika katika utunzaji wa wakazi, msaada na huduma kwa wakazi, na matengenezo na utawala. Hii ni pamoja na wafanyakazi wa uuguzi na utunzaji wa kibinafsi, wataalamu wa afya washirika, wafanyakazi wa utawala, jikoni, kusafisha, kufua na wa bustani.

### Je, ni lazima nimjulishe mwajiri wangu kama nimepokea chanjo ya COVID-19?

Hapana. Ni chaguo lako lakini unahimizwa kushiriki habari hii na mwajiri wako kama sehemu ya maandalizi ya COVID-19 na mipango katika kituo chako.

Mwajiri wako atatarajiwa kuwa na mazungumzo ya heshima na wewe ili:

- kueleza kwa nini anatafuta habari kuhusu chanjo za COVID-19 za wafanyakazi
- kuhakikisha unaelewa ni chaguo lako kupata chanjo ya COVID-19
- kuhakikisha unaelewa faragha yako italindwa, na
- kuhakikisha unajua haki yako ya kukataa kutoa habari hii.

### Je, ninahitaji kuonyesha ushahidi wowote wa chanjo yangu ya COVID-19 ikiwa niko tayari kushiriki habari hii na mwajiri wangu?

Hapana. Ni chaguo lako. Mwajiri wako atajadiliana nawe jinsi atakavyorekodi chanjo yako ya COVID-19, ikiwa uko tayari kushiriki habari hii nao. Kwa wafanyakazi ambao wako tayari, unaweza kutaka kupa mwajiri wako:

- cheti cha chanjo au ushahidi mwingine kutoka kwa mtoaji wa chanjo, au
- taarifa ya historia ya kinga ambayo unaweza kupata kutoka Medicare mtandaoni au programu ya simu ya Express Plus Medicare.

Unaweza pia kufikiria kutoa:

- tamko lililosainiwa au
- rekodi kutoka kwa mhudumu wa afya.

### Je! Naweza kupata habari wapi ili kunisaidia kuamua kuhusu kupata chanjo ya COVID-19?

Kituo chako kimepokea maelezo na vifaa vya kusaidia wafanyakazi katika kufanya uamuzi kuhusu kupata chanjo ya COVID-19, na kuwasaidia wafanyakazi kujua wapi wanapoweza kupata chanjo. Hii inajumuisha habari iliyotafsiriwa katika lugha 19. Unaweza pia kupata habari hii kwenye tovuti ya **health.gov.au**. Ni muhimu kupata habari zinazoaminika juu ya chanjo za COVID-19, kwa nini chanjo ni muhimu na jinsi ya kupata chanjo.

**Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na Idara ya Afya kwa Barua Pepe: AgedCareCOVIDLiaison@health.gov.au au wasiliana na chama chako cha wafanyakazi kupata ushauri na msaada.**